Kivu ya Kaskazini

# Mwanasiasa Nyamwisi kauwawa

Bwana Henoki Nyamwisi Muvingi, waziri wa zamani wa michezo pia wa utamaduni nchini mwetu ameuwawa kwa risasi siku ya ijumaa nne tarehe 5 januari 1993 pa Butembo katika mtaa wa Lubero.

Habari mbalimbali zilizotoka upande wa uko kaskazini ya jimbo, zaeleza *ya kuwa* bwana Nyamwisi ambae alirejea mtaa wa Beni siku *ya ijumaa* tatu, tarehe 4 januari akitokea Kinshasa, alikuwa akirudi Beni kusudi aitembelee mji wa Butembo upatikanao kunako kilometri 55 na Beni. Yasemekana ya kuwa wakati huo, marehemu Nyamwisi kawakutana waaskari walinda amani mikoani (gendarmes) ambawo walikuwa wanateka viongozi wa mji wa Butembo, nyara.

Viongozi hao *walikuwa wakifungwa baada ya askari* moja kuuwawa na wakaaji na kuzikwa na mavazi na viatu vyake vyote. Walipojulishwa hayo, waaskari walishikwa na hasira kali na kuwachukua viongozi wa mji na watumishi wawili wa msalaba mwekundu kusudi ya kuonyesha mahali hapo juu ya kumuondosha mwenzao shimoni na kumuzika kama ilivyostahili. Na wakati wa utafiti huo ndipo wakapambana na bwana Nyamwisi na walinzi wake. Tulijulishwa kwamba ilikuwa pembeni ya Posta ya Butembo kandokando ya makao ya kiongozi wa waaskari walinzi pale mjini Butembo. Ilielezwa ya kuwa wakati ule bwana Nyamwisi kawakaripia waaskari hao, akiwalazimisha kuwaachilia "wafungwa" wale na kuwaonya watiye silaha zao chini. Hapo hapo kukawa mizozo kati ya waaskari walinda amani na walinzi wa Waziri wa zamani, bwana Nyamwisi.

Bila kusita moja kati ya waaskari kachukua silaha yake kafyatula risasi kichwani na mwilini kote. *Waziri Nyamwisi kafa mara moja* na walinzi wake *kafungwa* kamba na kapelekwa ofisini mwa askari.Habari chache tulizozipata kwa njia kazaa zilijulisha eti maiti ya marehemu kabebwa kunako chumba cha wafu hospitalini hapo Butembo ambamo iliachwa hadi hapo *mapadri* na watu wengine kasihi wakuu wa askari kuiacha huru na kuipeleka mjini Beni ambako ilipaswa kuzikwa.

## Kifo cha ajabu na mshangao

Ingawa ukweli mkubwa ni kusema kama bwana Nyamwisi amefariki mchana kati kwa risasi ya waaskari walinda amani wa mji wa Butembo, kisa, namna na shida za kifo cha bwana Nyamwisi hazijulikane kawaida. Habari zenyi kutoka Butembo na Beni haziambatane kabisa. Watu leo husema kila mmoja nginsi alivyosikia. Tukichungua kwa karibu jambo hilo, twazani kama kifo hicho ni chenyi siri na vipenge vingi. Watu wote hufahamu kuwa tangu *demokrasia kafunguliwa* mnamo *tarehe* 24 Aprili 1990, ndugu huyo kajitangaza kuwa mpinzani wa raisi Mobutu na kuchagua chama cha D.C.F. cha profesa Ngoma Ngambu, ambamo katajwa makamu wake.

Wakati huo, bwana Nyamwisi katembelea majimbo mbalimbali nchini akijitetea mpaka kawa mwanasiasa bingwa mwenye kujulikana hasa zaidi jimboni mwa Kivu ya Kaskazini (Nord-Kivu), Kinshasa na hata Zaïre ya juu, na nchini Zaïre kwa jumla.Bwana Nyamwisi kawa waziri wa michezo katika serkali ya Profesa Lunda Bululu. Bila kukawia kajiuzulu na kuendelea na utetezi wake katika magazeti, redio na televisheni.

Wakati bwana Nguz a Karl I'Bond katajwa waziri mkuu, bwana Nyamwisi kawa waziri wa utamaduni. Mara tena kajiuzulu. Wakati ule, bwana Nyamwisi ambaye hakuwa tena katika chama cha D.C.F. kawa kama vile mwenyi kuitumikia jamaa la Raïsi wa Jamhuri (Mouvance présidentielle). Hata watu wengi kaanza kumuepuka na kumuogopa.

Jimboni mwa Kivu ya Kaskazini alishtakiwa na watu wengi kama mtu wa siasa ya kubagua kabila, kama vile Kyungu wa Katanga, wakati Liwali wa Jimbo, bwana Kalumbo Yohane-Petro na Prezidenti wa chama cha D.C.F./Nyamwisi wameanza kutunga vibarua vya kuogopesha wasiokuwa wazaliwa wa jimbo hili. Na hata kukusudia kuwafukuza jimboni wanainchi wa majimbo mengine. Ilisemekana kama siasa hiyo ya kuwatenga raia ni moja kati ya mipango ya bwana Nyamwisi.

Kwa upande mwengine, biashara na vifaa vya wafanyabiashara wa Beni, Butembo, Ishasha, Kiwanja, Rutshuru na Goma vimenyanganywa mnamo juma la tarehe 22 hadi 27 Desemba 1992 na waaskari-jeshi wa Rumangabo na wengineo pamoja na wakaaji wa mikoa hiyo. Yale yote yaliwekwa katika mzigo, bwana Nyamwisi na liwali wa jimbo aliye rafiki wake tena mwanamemba wa chama chake cha D.C.F.

Kabla ya kuuwawa, bwana Nyamwisi kajulisha Redio-Virunga ya Goma, eti ni wakuu wa waaskari jimboni ndio kawaruhusu majeshi yao kuiba mali na biashara ya wafanyabiashara wa jimbo la Kivu ya Kaskazini. Bwana Nyamwisi kashambulia pia kunako redio "Bakuyakuya" na kahaidia kuleta siasa ya kuwasahisha. Matangazo yale kwenye redio kapiga watu bumbwazi mkuu na wakati watu walikuwa wanafikiri kuhusu masemi ya Nyamwisi, ndipo wamepata habari ya kifo chake siku mbili baadaye. Nani aliyemua Nyamwisi? Ni kwa nia ya yule askari pekee ao ametumwa na watu wengine ?

Kifo chake ni kifo cha msiba ao cha kisiasa ? Bwana nyamwisi amefariki juu ya nini ? Ndio maswali yenyi kuzunguusha vichwa vya wakaaji wa jimbo la Kivu ya Kaskazini.

Tutajulisha pia kwamba marehemu Nyamwisi amezikwa mbele ya jamaa lake. Liwali Kalumbo na mdogo wake kaogopa kuwa waweza kuuwawa nao. Bwana Nyamwisi kafariki kwa umri wa miaka 42, kaacha mke mjane na watoto yatima.

Uwoga wasumbua leo watu wote. Watu wamekimbia mji wa Butembo. Nyumba zimeunguzwa, askari wamejielekeza Kasindi, wengine wajaa mjini Goma. Kwa heri Nyamwisi, roho yako itulie, ukae na Bwana Mungu. Unaenda kijana, vijana wenzako watakuombea kwa maisha yako ya milele.

**Gabriël Lukeka bin Miya**

## JE, UMESIKIA ...

***Kama,***
liwali wa jimbo la Kivu la Kaskazini kawapiga bumbwazi maprezidenti wa vyama vya kisiasa ? "Ninayo majeshi miongoni mwangu ". Kwa kweli hakuna hata mtu moja aliweza kusadikia mambo kanena liwali wa kivu ya kaskazini wakati wa masimulizi kawa nayo na maprezidenti wa vyama vya kisiasa siku hiyo. Kwa kushuhudia oni hilo, askari-jeshi kamuonyesha cha mtema kuni wakati wa fujo iliyozuka jimboni. Uwizi, ujeuri na vinginevyo vitendo haramu kafanywa kaonya ukweli upi. Hasa wakaaji, huko, walikuwa wakinongoneza kuwa wafuasi wa Rumeo, akida wa askari-jeshi, walikuwa wakitamani kurudi kufanya mzozo akiweko msafani wa mbele bwana Kalumbo ambaye kadai hakuna uhuni wowote huko. Ebu ! Kumbe wazo silo kitendo ?

***Kwamba,***
kundi moja la wanafunzi kashtaki uongozi wa univasti "ULPGL" ya Goma ? Eti kundi hilo la wanafunzi baada ya kutishwa na ukosefu wa haki katika hatua kazaa kachukuliwa juu yao na ambayo kaonekana kuwa kali na mmoja kati ya viongozi. Yasemekana huko kuwa ubaguzi wafanyika wakati wa mitihani kulingana na hali ya wanafunzi. Majibu kwa maulizo siyo ya lazima bali sura ya kike ndiyo yawapevusha wanaohusika. Na huko mahakamani haijulikane hukumu itachukuliwa je ingawa waamzi ni walimu pia kunako Univasti hiyo ambako walipwa mishahara kwa feza za ujeremani. Kwa ngambo yao, viongozi wa shule hilo waomba walipwe zaïre miliari 12 kama vile kodi kwa mashtaka hayo ya uwongo, wasema : Loo ! isiwe tu Univasti hiyo "ULPGL", bali pia mjini Bukavu wanafunzi wa chuo cha "ISGEA" kafanya mgomo wa kusoma kutokana na malipisho yafanyika kwa feza nyingi za kigeni wakati wajiandikisha na kwa kuruhusiwa kusoma. Samani ya feza yafikia kiasi cha mamia ya milioni ya feza zaïre. Hum !

***Eti,***
ulimwengu ni kwa wale walio werevu katika mambo yote ? Waganga mjini Goma kayakumbuka na kufanya ili kujipatia feza bila kujali ugonjwa wa "méningite" ulioko mipakani mwetu. Baada ya kuuza chupa za ndui ya "méningite" kwa bei ya franka 100.000 za kirundi kwa jumla ya watu 50 (watu hao wa Goma kawalazimisha kila mkaaji milioni 6) na kuona watu kama vile nyama watumishi wa mashirika miongoni mwao wakiweko wakaaji. Kitendo hicho bila kukubaliwa na chumba cha afya jimboni kaonekana halali sababu wakuu huko hawakuweza kufanya lolote. Ugonjwa huo, umekwisha kuonyesha matukio yake na kuwauwa watu mjini Bukavu. Ni kweli kusema kama uchuuzi wafaa kuliko afya ya watu sio uwongo katika dunia hii ya sasa.

***Kuwa,***
baada ya kuzomewa na watumishi wake mjini Kalemie, kiongozi mkuu wa shirika la SFE karudi mikono mitupu mjini Kindu baada ya kupitia mji mkuu Kinshasa ? Kiongozi huyo hajui tena ginsi ya kuliongoza shirika lake. Yasemekana pia kama wafanyakazi wasiopendelea kutoka Kalemie hawakubali tena mwito wake kwa njia ya vibuu vya anga. Na wakati huu wafanyakazi wa Kindu wapendelea kugoma kazi mpaka hapo mfanyakazi wa ngazi ya chini tapokea milioni 50 ya zaïre sawa wenzio wa Kalemie. Kumbe hakuna anayeongoza shirika la SFE huko.

***Kama,***
kwa ajili ya kuzuia fujo izukapo wakati wowote mjini Kindu jimboni Maniema, liwali Omari Lea SISI kawachukua kazini vajana yapata 100 toka mitaa ya mji ? Baada ya kupokea kila moja wao yapata zaïre milioni 3 na mia 5 sawa pesa ya kuwakaribisha kazini, vijana hao watahusika na kulinda amani, alivyosema liwali huyo asiyeaminiwa tena kunako jumba la maburudiko la SFE. Kwa upande wa wanasiasa wapendao mabadiliko, vijana hao kateuliwa kwa manufaa ya matayarisho ya uchaguzi wa raïs siyo ya kulinda amani. Yawezekana je katika nchi iliyo na uhuru na yenye haki kuendesha mambo kama hayo ?

Kivu ya Kusini

# Sikash yaendelea kuhusika na afia ya wakaaji

Kutokana na magumu mengi kapata wamama kwa kuzaa kama ifaavyo, shirika Sikash ambalo lahusika na miradi mbalimbali kwa maendeleo ya mkoa wa Kasha lilijitahidi kufungua kitua cha matibabu hapo Mushekere. Kituo hicho kitahusika zaidi na mama pia watoto. Sherehe za ufunguo wake ziliongozwa na myampara wa mji wa Bukavu, bwana Christophe Migale Mwene Malibu Nabulizi mnamo tarehe 23 desemba 1992. Kati ya waalikwa kulikuweko, mganga kiongozi mkuu wa jimbo la Kivu ya Kusini, daktari Kabi Dibi-Dibi, mganga kiongozi wa mtaa wa afia wa Bukavu, daktari Kabongo Mutuapikay, kiongozi wa mtaa wa Bagira, bwana Tabaro, kiongozi wa mradi kuhusu ukadirisho wa uzazi, bwana Mbwiliza, wakuu wengi pamoja na umati wa wakaaji waliokuja kusherehekea siku hiyo.

Katika hotuba zilizotamkwa ilionywa kuwa kituo hicho kilikuwa cha lazima sana. Kwani wamama wengi wa Kasha walilkuwa wakizala nyumbani. Kwa kuwa hospitali zapatikana mbali na makwao. Kuzaa nyumbani yaonya hatari nyingi ambazo sisi wote twaweza kujua. Kutokana na matatizo yaliyoko, wamama kaomba kwa shirika Sikash kutafuta majawabu. Ni hivi likisaidiwa na wanamemba wake, mashirika mengine na wote wenyi utashi mwema, misaada katolewa kafikilia ukomo wa mradi kachukuliwa. Kwani kusimikwa kwa kituo hicho itarahisisha kiasi magumu kawa nayo akina mama na watoto kuhusu afia yao. Hiyo ni alama kweli yaonya kuwa shirika Sikash yahitaji kuiinua maisha ya wanamemba wake na maendeleo ya mahali wakaa. Kituo hicho kitaongozwa na akina bibi Astrida Nabintu akisaidiwa na dada waganga Aimé Cirezi na Salumu Awezae na wengineo watumishi kazaa.

Ingawa shirika hilo lajitatahua kupinga magumu yaikumba umma, watu wasio na zamiri ya kuendelesha makwao waendelesha vitendo visivyolingana na ujenzi bora wa nchi. Kwani warugaruga wamoja walijiruhusu kuiba singa za moto wa stimu ambazo zilisimikwa kwa kuuchukuwa moto huo hadi kituo hicho.

Bali pia wayanguyangu hao kaongoa mirija kawekwa kwa kufikisha maji safi kwenyi kituo hicho pia. Ni toka vitendo hivyo haramu ilombwa kwa wakaaji waamshe zamiri yao ya kuipenda nchi yao na raïa waishimo hasa mkoani Kasha ambako migongano kwa wakaaji wabadilishe na kutupilia mbali tabia zao mbaya. Wapendane na waheshimu mali ya umma kwa manufaa yao wenyewe.